



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA



Kumb. Na.MDC/L.20/6/VOL.LXXXVI/32

9/11/2023

Mkurugenzi Mtendaji
Kituo cha Uwekezaji Tanzania
S.L.P.938,
Dar Es Salaam.

YAH: KUWATAMBULISHA KAMPUNI YA VINDA INDUSTRIAL LIMITED
WILAYA YA MKURANGA


Rejea mada tajwa hapo juu,

Ninachukua fursa hii kuijulisha Ofisi yako kwamba, kampuni tajwa hapo juu imenunua kipande cha Ardhi kutoka kwa Rajabu Ramadhani Holea Kijiji cha Msufini Kidete lenye ukubwa wa ekari kumi. **Kampuni ya Vinda Industrial Limited ya S. L. P. 11858, Dar es salaam** ni Kampuni ya uwekezaji kutoka nje ya nchi, ambayo imenunua Ardhi kutoka kwa mwananchi ikiwa ni Ardhi ambayo bado haijapimwa, taratibu za kupanga matumizi na kasha kupima Ardhi hii zinaendelea kufanyika.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999, fungu la 20 sambamba na Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na. 26 ya 1997, Ardhi hii kabla na baada ya upangaji na upimaji linatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), aidha kwa kuzingatia fungu la 12 & 179 Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 na Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, Kanuni za Ardhi za 2001 kanuni ya 9C (v), nawasilisha utambulisho huu ili taratibu za kuwatambua na kuwasajili ziendele.

Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi kwako ili iweze kupatiwa Certificate of Incentive ambapo baada ya upimaji cheti hiki kitafanyiwa marekebisho kuonesha namba ya kiwanja uwekezaji utakapofanyika.

Naomba kuwasilisha.


Chagiye RM,
K.n.y: Mkurugenzi Mtendaji (W),
Mkuranga.

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W)
Mkuranga